## Umuhimu wa Mafunzo ya Ndoa

- Huongeza maarifa na ufahamu kuhusu Taasisi ya Ndoa.
- Huongeza ufanisi katika utendaji kazi na kujiamini kwa mwanandoa.
- Huimarisha afya bora ya mwanandoa na ustawi wa familia.
- Hujenga na kuimarisha uhusiano wa wanandoa.
- Husaidia kufahamu Nafasi, Haki na Wajibu katika Ndoa.
- Husaidia vijana wanaotarajia kuoa au kuolewa kujitambua.
- Vijana kuwezeshwa kufanya maamuzi sahihi kwa wakati sahihi kuhusu Ndoa.
- Humuandaa kijana kuwa mume au mke bora.


## Matokeo Chanya Baada ya Mafunzo ya Ndoa

- Uhusiano Ulioimarika na Wenye Mvuto.
- Uwajibikaji katika Ndoa.
- Uwapo wa Furaha, Amani na Utulivu katika Ndoa.
- Malezi bora kwa Watoto.





**For Training, Counseling and Guidance Contact us:**
Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare)
P. O. Box 185, Bong'wa Street,
Bagamoyo, PWANI, Tanzania
**Phone:** +255 744 000 066
**Email:** info@tamcare.or.tz
**Website:** www.tamcare.or.tz



# MAFUNZO YA NDOA

## Utangulizi

- Ndoa ni taasisi nyeti na muhimu katika maisha ya binadamu. Ni Taasisi muhimu katika Nyanja zote za dini, jamii, serikali na siasa. Bila kuwa na ndoa nzuri na imara, dini, jamii, serikali na hata siasa vitayumba na kukosa maadili mema, haki, utulivu, na amani miongoni mwa watu.
- Ni jambo la kusikitisha kuwa, watu wengi wanaichukulia taasisi ya ndoa kwa wepesi. Watu hawajiandai ipasavyo kwa ajili ya maisha ya ndoa. Matokeo yake ni mpasuko na kuvunjika kwa ndoa nyingi.
- Utafiti umeonesha kuwa matukio ya wanandoa kuachana yameongezeka Nchini. Tafiti zilizowahi kufanywa na asasi isiyo ya kiserikali ya Wanawake Wanasheria (WLAC) na Chama cha Waandishi Habari Wanawake (TAMWA) zilibaini kuwepo kwa ongezeko la visa vya wazazi wanaotengana kutoka 2,390 mwaka 2005 hadi visa 4,349 mwaka 2006. Kwa mujibu wa taarifa za baadhi ya ofisi za Idara ya Ustawi wa Jamii wilayani, kuna wazazi wanandoa au walio kwenye mahusiano kati ya 36 na 45 wanaotoa taarifa za kutengana na kutafuta usaidizi wa kuwalea watoto kila mwezi.
- Kwa mujibu wa taarifa za maafisa polisi kwenye madawati ya kijinsia katika wilaya mbili za mkoa wa Dar es Salaam, visa 11 hadi 17 hutiripotiwa kila mwezi.
- Kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2008/09, kiwango cha talaka kilikuwa asilimia 1.1 lakini mwaka 2011/12 kilipanda hadi asilimia 1.2. Mwaka 2014/15, takwimu zinaonesha kuwa kilikuwa asilimia 2.1 na mwaka 2017/18 kilipanda hadi asilimia 2.9. Sambamba na takwimu hizo za talaka, pia ilielezwa kuwa wanandoa 232,415 waliohojiwa walibainisha kuwa wanaishi wakiwa wametengana na wenzi wao. Taarifa hiyo ambayo ilinukuliwa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ilibainisha kuwa wanandoa 715,447 waliachana kwa talaka.
- Taarifa ya Waziri wa Sheria na Katiba Nchini ya Tarehe 17 Aprili 2019 aliyotoa Bungeni, pamoja na mambo mengine, Waziri alibainisha kuwa, idadi ya ndoa 26,953 na talaka 122 zilisajiliwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019. Hii inamaanisha kuwa, kila mwezi kuna talaka 14 zinazosajiliwa Nchini sawa na Talaka moja (1) kila baada ya siku mbili (2). Baadhi ya ndoa zimedumu muda mfupi chini ya mwaka mmoja
- Hizi ni ndoa zilizosajiliwa. Ziko ndoa ambazo wanandoa wameamua kuzivunja wenyewe bila kuzingatia taratibu na sheria za Nchi kuhusu Ndoa, hivyo, taarifa zao haziko RITA. Wako wanandoa ambao wametengana na mashauri yao bado yako mahakamani. Wako wanandoa wanaoishi pamoja ili kulinda heshima ya ndoa, lakini hawana mahusiano mema na wala mawasiliano.
- Hali hii ni sehemu ya visababishi vya ongezeko la wazazi wasio na wenza (single parents) Nchini. Hii ni changamoto kubwa inayoikabili nchi yetu. Athari zake ni kubwa kwa watoto waliozaliwa katika ndoa hizo, wazazi wenyewe,familia zilizozalisha wanandoa, jamii na Taifa kwa Ujumla. Ongezeko la watoto wa mitaani na wanaoishi katika mazingira magumu, ukatili kwa watoto, watoto waliokosa maadili mema, walioacha shule, walioathirika kiafya na kisaikolojia, waliojiingiza katika vitendo vya uhalifu kama vile kula madawa ya kulevya, umalaya, ujambazi na makosa mengine ya kijinai ni sehemu ya matokeo ya hali kama hii.
- Ndoa ni kitovu cha malezi na ustawi wa jamii na Taifa. Ni taasisi muhimu ya kujenga upendo, amani, na mshikamano. Hivyo, ili kuwa na jamii na Taifa lenye ustawi na maendeleo ni muhimu Ndoa kuwa imara na zenye furaha. Ndoa zisizo na furaha, huathiri afya ya mtu binafsi, ustawi wa familia, jamii, Taifa na ufanisi katika utendaji kazi.



## TaMCare ni Nini?

Asasi ya Ndoa na Malezi kwa Watoto Tanzania, yaani Tanzania Marriage and Child Care Foundation, kwa kifupi TaMCare, ni Asasi isiyo ya Kiserikali na isiyo ya kutafuta faida yenye makazi yake Wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani katika Tanzania Bara. Asasi hii imesajiliwa na Serikali Mwezi Oktoba mwaka 2019. Namba yake ya usajili ni 00NGO/R/0717.

## Dira Yetu

Kuwa taasisi bunifu na inayoaminika katika kuchangia uwepo wa jamii bora inayotokana na ndoa imara na malezi bora kwa watoto.

## Dhima Yetu

Kutoa huduma bora na endelevu kuhusu ndoa na malezi bora kwa watoto kwa njia ya kutoa elimu, ushauri na unasihi, na mbiu shawishi ili kuwa na familia na jamii bora kwa maendeleo ya Taifa la Tanzania.

## Wanufaika Wakuu wa Mafunzo Yetu

- Wanandoa
- Wanandoa Watarajiwa
- Vijana wa Kike na Kiume.